SIKU 16 ZA UANAHARAKATI

# KAMPENI YA SIKU 16 ZA UANAHARAKATI DHIDI UKATILI WA KIJINSIA, 2022

**Kila Uhai Unathamani!**
**Tokomeza Mauaji Na Ukatili Dhidi Ya Wanawake Na Watoto**

## 1.0 UTANGULIZI

Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia ni kampeni kabambe ya kimataifa iliyoanzishwa na Kituo cha Kimataifa cha Wanawake katika Uongozi "Women's Global Leadership" tokea mwaka 1991.

## 2.0 CHIMBUKO LA KAMPENI

Chimbuko la kampeni hii inatokana na vuguvugu la wanaharakati duniani kupaza sauti kukemea vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia. Wanaharakati wengi barani Ulaya, Amerika, Asia na Afrika walijenga nguvu ya pamoja na kuleta msukumo wa kutambulika na kuheshimika haki na ulinzi wa wanawake ili kupunguza vitendo vya ukatili walivyokuwa wakifanyiwa wanawake. Mathalani, mauaji ya kinyama ya wanawake wa Mirabelle yaliyofanyika nchini Dominica mwaka 1960. Kuanzia Novemba 25 mwaka 1991, Umoja wa Mataifa ulitenga siku hii kama siku ya Kimataifa ya kutokomeza Ukatili dhidi ya wanawake.

Kampeni ya siku 16 za Unaharakati Dhidi ya Ukatili wa kijinsia huishia Disemba 10 ambayo ni Siku ya Kimataifa ya Tamko Rasmi la Haki za Binadamu, ikiwa ni ishara ya kuhusisha ukatili dhidi ya wanawake na haki za binadamu na kutia msisitizo kwamba ukatili kama huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Ndani ya siku hizi 16 za kampeni ya uanaharakati kuna tarehe za siku zingine za Kimataifa ambazo ni muhimu katika kulinda haki za wanawake. Tarehe hizo ni pamoja na Novemba 29 ambayo ni Siku ya Kimataifa ya Watetezi wa Haki za Binadamu Wanawake, Disemba 1 Siku ya UKIMWI Duniani, Disemba 3 Siku ya watu wenye ulemavu, Disemba 6 Siku ya kukumbuka mauaji ya kikatili ya Montreal 1989 ambapo Wanawake 14 waliokuwa wanasomea uhandisi waliuawa na mtu aliyekuwa anawachukia wanawake na Disemba 10 Siku ya Tamko Rasmi la Haki za Binadamu. Hivyo basi, siku hizi 16 zinatoa mwanga na msukumo kwa watu, Serikali, jamii na mtu binafsi kutambua kwamba ukatili dhidi ya wanawake ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

WiLDAF TANZANIA

MKUKI UKATILI

Siku hizi 16 za uanaharakati dhidi ya Ukatili wa Kijinsia zimekuwa zikitumiwa na wadau ulimwenguni kote kama mbinu mahsusi za kutoa wito kwa jamii ili kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike kwa kufanya yafuatayo:-

1. Kujenga uelewa kuhusu ukatili wa kijinsia kama uvunjaji wa haki za binadamu kijamii, kitaifa, kikanda na kimataifa.
2. Kuimarisha kazi za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake katika ngazi za chini na kujenga daraja kati ya kazi za maeneo mbalimbali yanayofanya Ukatili dhidi ya wanawake kama nyenzo ya kuwa kwamua kiuchumi.
3. Kubadilishana taarifa na uzoefu kuhusu Ukatili dhidi ya wanawake kati ya wadau.
4. Kuonyesha mshikamano ulimwenguni kote kutokomeza Ukatili dhidi ya wanawake.
5. Kutumika kama chombo cha kupaza sauti ili wadau wote waweze kutekeleza wajibu wao katika kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake.
6. Kuwajibisha mamlaka husika kutekeleza ahadi za kuzuia na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia

Kama ilivyo katika nchi zingine za Afrika, vitendo vya ukatili wa kijinsia hapa Tanzania,vimekuwa vikiongezeka kwa kasi kubwa. Ukatili huo unajidhihirisha katika namna mbalimbali ikiwemo vipigo, ukeketaji, ubakaji, mauaji ya wanawake na watoto wa kike, kurithi wajane, ukatili nyumbani, ukatili dhidi ya wenza, ukatili wa mitandaoni, ukatili dhidi ya wanawake kwenye siasa, ukatili dhidi ya wanawake katika chaguzi, ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake katika ulimwengu wa kazi na rushwa ya ngono.

Ukatili una athari mbaya kwa wanawake wenyewe, watoto na kwa jamii, kwani huathiri afya zao kimwili na kisaikolojia na hivyo hupelekea kudidimiza maendeleo yao na ya taifa kwa ujumla wake.

**Uzoefu wa Maadhimisho ya Siku 16 za Uanaharakati Dhidi Ukatili wa Kijinsia Kimataifa**

Nchini Tanzania, WiLDAF kama mtandao kwa kushirikiana na wanachama wake kama vile LHRC, WLAC, TAMWA, na TGNP walianza kuazimisha kampeni hii tangu mwaka 1996. Baadae (2011) uliundwa Mtandao wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia (MKUKI) chini ya uratibu wa WiLDAF. Mtandao huu umekuwa ukiongoza kampeni hii ya Siku 16 za Uanaharakati kwa kushirikiana na Serikali, mashirika mengine yasiyo ya kiserikali, wadau wa maendeleo pamoja na sekta binafsi ili kuleta nguvu ya pamoja kutokomeza vitendo vya Ukatili wa Kijinsia.

Aidha viongozi mbalimbali wa kitaifa wameshiriki kama wageni rasmi katika uzinduzi wa Siku 16 za Uanaharakatidhidi ya Ukatili wa Kijinsia. Viongozi hawa ni pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mheshimiwa Mary Nagu akiwa Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Sophia Simba akiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margreth Sitta akiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto,Dkt. Asha Rose Migiro akiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Mheshimiwa Angela Kairuki akiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na akiwa Waziri wa Uwekezaji, Mheshimiwa Ummy Mwalimu akiwa Waziri wa Afya, Wazee Jinsia na Watoto na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

Ushiriki wa Viongozi hawa pamoja na wengine umeongeza ushirikiano wa serikali na asasi za kiraia katika mapambano dhidi ya Ukatili wa Kijinsia.

SIKU 16
ZA UANAHARAKATI

Kauli mbiu

Zifuatazo ni kauli mbiu mbali mbali zilizotumika kwenye maadhimisho yakampeni ya Siku 16 za KupingaUkatili wa Kijinsia.

| | |
|---|---|
| 1991- 1992 | Ukatili Dhidi ya Wanawake huvunja haki za binadamu |
| 1992- 1993 | Demokrasia bila haki za Wanawake siyo Demokrasia. |
| 1994 | Ufahamu, Uwajibikaji, Vitendo: Ukatili Dhidi ya Wanawake huvunja haki za Binadamu. |
| 1995 | Vienna, Cairo, Copenhagen na Beijing: Inaleta Haki za Wanawake Nyumbani. |
| 1997 | Dai haki za Wanawake Nyumbani na Ulimwenguni Kote. |
| 1998 | Kujenga Utamaduni wa Kuheshimu Haki za Binadamu. |
| 1999 | Kutimiza Ahadi ya Uhuru Dhidi ya Ukatili. |
| 2000 | Kusherehekea miaka 10 ya Kampeni. |
| 2001 | Ubaguzi na Ujinsi:Maliza Ukatili. |
| 2002 | Kuunda Utamaduni Unaokataa Ukatili Dhidi ya Wanawake. |
| 2003 | Ukatili Dhidi ya Wanawake huvunja Haki za Binadamu. Kuendeleza yatokanayo na Mkutano wa Vienna. |
| 2004 - 2005 | Kwa Afya ya Wanawake, Kwa Afya ya Ulimwengu; Acha Ukatili. |
| 2006 | Sherehekea Miaka 16 ya Siku 16; Endeleza Haki za Binadamu – Komesha Ukatili Dhidi ya Wanawake. |
| 2007 | Madai ya utekelezaji, mapambano na changamoto dhidi ya vikwazo ili kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake. |
| 2008 | Haki za Binadamu za Wanawake ni Haki za Binadamu Wote: Sherehekea Miaka 60 ya Tamko Rasmi la Haki za Binadamu” |
| 2009 | “SIKO PEKE YANGU - Mwenye nia Binafsi, Uthubutu na Utayari wa Kuzuia na Kupambana na Ukatili wa Kijinsia |
| 2010 | “Pinga Ukatili Kuimarisha Familia”. |
| 2011 | “Miaka 50 Ya Uhuru: Pinga Ukatili WaKijinsia Kuimarisha Tanzania Huru |
| 2012 | “FUNGUKA! Kemea Ukatili Dhidi Ya Wanawake. Sote Tuwajibike” |
| 2013 | “FUNGUKA! Tumia Mamlaka Yako, Zuia Ukatili Wa Kijinsia: Boresha Afya Ya Jamii” |
| 2014 | FUNGUKA! Pinga Ukatili wa Kijinsia kwa Afya ya Jamii. |
| 2015 | FUNGUKA! Pinga Ukatili Wa Kijinsia: Elimu Salama Kwa Wote |
| 2016 | FUNGUKA! Pinga Ukatili Wa Kijinsia: Elimu Salama Kwa Wote. |
| 2017 | “FUNGUKA! Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto Haumuachi Mtu Salama. Chukua Hatua” |
| 2018 | FUNGUKA! Usalama Wake; Wajibu Wangu. |
| 2019 | Kizazi Chenye Usawa: Simama Dhidi ya Ubakaji |
| 2020 | Mabadiliko Yanaanza na Mimi! |
| 2021 | Ewe Mwananchi! Komesha Ukatili wa Kijinsia Sasa |

## 3.0 MAFANIKIO

1. Kuongezeka uelewa kwa jamii juu ya athari za ukatili wa kijinsia na haja ya kushiriki kwenye kuchukua hatua kukomesha ukatili wa kijinsia. Kupitia kwa wadau mwitikio umekuwa mkubwa na watu wengi zaidi wanajitokeza kuongea, kukemea na kutetea kwa uwazi juu ya ukatili wa kijinsia.
2. Kuongezeka kwa ushirikiano baina ya Serikali na wadau katika kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake. Hali hii imepelekea msukumo wa uboreshaji, utengenezwaji na utekelezwaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Vitendo vya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).
3. Kuongezeka ufanisi na kuwepo mpango mkakati wa kuratibu na kusimamia vituo vya kutoa msaada wa kisheria ili kuhudumia watu waliofanyiwa ukatili na dhuluma mbali mbali ikuimarishwa zaidi.
4. Kuongezeka kwa mbinu bunifu za kupambana na ukatili wa jinsia kwa asasi zinazofanya kazi ndani ya jamii ikiwemo ujumuishi wa wanaume na walezi wa watoto.
5. Kuongezeka kwa utoaji wa taarifa za ukatili kwa wanawake na watoto.
6. Kuongezeka kwa ulewa mkubwa kuhusiana na kampeni ya siku 16 za uanaharakati dhidi ya ukatili wa kijinsia pamoja na kuwa na mwamko kwenye kuazimisha kampeni.

## MALENGO YA KAMPENI 2022

Kwa kuangazia hali halisi ya matukio ya ukatili wa kijinsia na kauli mbiu za kimataifa, Kampeni ya mwaka huu ina malengo makuu yafuatayo;

1. Kushawishi utungwaji Sheria Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia kama inavyopendekezwa na Sheria ya Mfano ya SADC (SADC Model Law on GBV);
2. Kuhamasisha haja ya mamlaka kuongeza ushiriki wa wanawake na wasichana katika nafasi za uongozi na maamuzi ya kisiasa na kisera; Ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua kuzuia ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na uchaguzi.
3. Kuimarisha sauti za wafeminia na wanaharakati wanawake katika kazi zao mbalimbali za kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake;
4. Kuhamasisha kila mtu kujiunga na harakati za Kupinga Ukatili Dhidi ya wanawake na Watoto katika Jamii zao wakati wote wa kampeni na baada ya kampeni.
5. Kusherekea mafanikio tuliyofikia kama MKUKI ya kupambana na ukatili wa jinsia na kuendelea kutambua juhudi za mtu mmoja mmoja, kundi pamoja na Serikali katika kupambana na ukatili wa jinsia.

## NINI CHA KUFANYA KIPINDI CHA KAMPENI

Ukatili wa kijinsia upo na unafanyika katika maeneo ambayo tunayafahamu na tunayashuhudia. Wanaofanya vitendo hivi ni watu ambao wanafahamika na jamii kama vile, walezi, wazazi, wapenzi na wenzi wa ndoa. Madhara ya ukatili ni makubwa na yanaweza kupelekea vifo. Mathalani, Matukio mengi ya mauaji dhidi ya wanawake yamekuwa yakitokea kwenye mahusiano yenye migogoro iliyogubikwa na vipigo vya mara kwa mara. Jamii imekuwa ikishuhudia pasipo kuingilia kati na kutoa msaada. Wakati mwingine jamii imekuwa ikishiriki kusuluhisha migogoro ya vipigo badala ya kutoa taarifa polisi. Kwa hali hii ni wazi kuwa, iwapo jamii itabadilika na kushiriki kikamilifu kwenye harakati za usawa wa kijinsia ni dhahiri vitendo vya mauaji dhidi ya wanawake vitatokomezwa kabisa.

Kuwa sehemu ya mabadiliko, ungana nasi kuzuia na kutokomeza vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia kwa kufanya yafuatayo;
Mtu binafsi;

**Badilika usifanye vitendo vya ukatili:** Kumbuka kwamba ukatili wa kijinsia ni kosa kisheria.

**Kemea vitendo vya ukatili:** Unaposhuhudia vipigo, unyanyasaji, ukatili wa aina yoyote nyumbani kwako au jirani, chukua wajibu kukemea na kuchukua hatua dhidi ya vitendo hivyo.

**Toa Taarifa za Ukatili:** Unaposhuhudia au kufanyiwa vitendo vya ukatili, toa taarifa kwenye mamlaka mbalimbali kama vile Polisi hususani madawati ya jinsia, Ofisi za Serikali za Mita, Wasaidizi wa Kisheria walio karibu na wewe na kwa maafisa wanaoshughulikia masuala ya ustawi wa jamii.

**Elimisha jamii juu ya athari za ukatili:** Unaweza kujifunza na kuanzisha mijadala mbali mbali kwenye jamii yako juu ya athari za ukatili, kupita vijiwe vya boda boda, vijiwe vya kahawa, sehemu za michezo, masokoni, sehemu za ibada na sehemu nyingine yoyote ambayo wewe unafanya kazi zako za kila siku.

## KILA UHAI UNATHAMANI!
## TOKOMEZA MAUAJI NA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO

### JAMII

Je jamii inawajibu gani katika kuhakikisha wanawake na watoto wanakua salama?

**OKOA MAISHA:** Jamii zinaweza kuendelea kufanya kazi katika kupambana na ukatili kwa kusaidia na kuhimizana katika kulinda wanawake na watoto katika ngazi ya jamii, kwa kufanya yafuatayo;

Kuunda Kanuni za kuchukua hatua kwa wahalifu wa ukatili. Kwa kupitia mikutano ya kijamii, jamii inaweza kuunda kanuni za kuwachukulia hatua watu wote wanaofanya ukatili  ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa na ufuatiliaji wa kesi husika.

Jamii inapaswa kutoa ushirikiano na vyombo husika wakati wa uchunguzi na kutoa Ushahidi: Jamii inaposhuhudia vitendo vya ukatili inapaswa kutoa ushirikiano kwa vyombo husika kutoa ushahidi ili wahusika waadhibiwe kisharia. Jamii inapaswa kukumbuka kwamba swala la ukatili sio swala binafsi la kifamilia kwa sababu linathiri jamii nzima.

Viongozi wa dini, viongozi wa kimila, watu mashuhuri na viongozi wa kijamii kwa kutumia majukwaa yao kuongea kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia  kwa sababu wanaaminika wanaweza kubadili mtazamo wa jamii juu ya vitendo hivyo. Vile vile kutumia tafsiri za maandiko ili kuhakikisha wanawake wanakua saw ana wanaume katika kufurahia fursa katika kijamii.

### SERIKALI

Je, kuna sera na sheria madhubuti dhidi ya vitendo vya Ukatili? Je kuna mifumo wezeshi ya utoaji wa taarifa na msaada kwa watendewa wa vitendo vya Ukatili?

**OKOA MAISHA!** Boresha mazingira salama ya kisera na kisheria katika kuzuia na kutokomeza ukatili majumbani, kwa kufanya yafuatayo;

Kuhakikisha Uundwaji wa Sheria Maalumu ya Ukatili: Serikali inapaswa kuandaa Sheria maalumu ya Ukatili.

Kupitia Upya Sheria na Sera: Serikali inapaswa kupitia upya sheria zote zinazokinzana na kuzifanyia marekebisho ili kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa vifungu vya kisheria ili kukomesha ukatili